**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**PRESIDENT'S OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

**NZEGA DISTRICT COUNCIL**


All correspondence should be addressed to:

MKURUGENZI MTEND. HALMASHAURI YA WILAYA NZEGA.

District Executive Director,
P.O Box 4,
**NZEGA**

Tel: +25526 269 2349
**Email: md@nzegadc.go.tz**
**Website: www.nzegadc.go.tz**


REF: NDC/~~MV~~.S.2/8A/09........ **26.10.2021**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MKATABA

**Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri ya wilaya ya Nzega kwa kushirikiana na shirika lisilo la kiserikali la MDH anawatangazia watu wote wenye sifa kuomba nafasi za kazi za mkataba wa mwaka mmoja katika fani zifuatazo:**

### 1.0 MUUGUZI MSHAURI DAWA (ART NURSE) – NAFASI 10

#### 1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

I. Mwombaji anatakiwa awe na elimu ya kidato cha Nne (IV) au cha sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya stashahada (Diploma) ya Uuguzi au zaidi.

II. Mwombaji lazima awe na leseni ya uuguzi iliyo hai ambayo imetolewa na Mamlaka husika.

#### 1.2 SIFA ZA ZIADA/UZOEFU

Wenye uzoefu wa kuanzia mwaka mmoja au zaidi katika fani husika.

#### 1.3 KAZI / MAJUKUMU YA MUUGUZI MSHAURI DAWA (ART NURSE)

I. Kuhakikisha anatoa huduma kwa kufuata sheria na maadili ya Uuguzi

II. Kuhakikisha huduma zinatolewa kwa ufanisi katika kituo cha kutolea huduma

III. Kuhakikisha wateja wote wanapata majibu ya uchunguzi ya maambukizi ya VVU kwa kufuata kanuni.

IV. Kuhakikisha wagonjwa wanapata huduma sahihi kila wanapotembelea kituo cha kutolea huduma, iwe kwa kufuata ratiba au bila ratiba.

V.Kutoa ushauri kwa wateja mara baada ya kupata majibu.

VI. Kuhakikisha taarifa zote zipo sahihi kila wateja wanapofika kwenye kituo cha kutolea huduma.

VII. Kutoa ushauri katika ngazi ya familia juu ya umuhimu wa kuwahi katika vituo vya kutolea huduma za afya.

VIII. Kufanya kazi zingine atakazopangiwa na msimamizi wake wa kazi.

IX. Awe tayari kufanya kazi na kuishi katika mazingira yeyote hasa vijijini

## 2.0 MFUATILIAJI WATEJA KATIKA KLINIKI ZA TIBA NA MATUNZO (CLINICAL TRACKER) – NAFASI 3

### 2.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Mwombaji anatakiwa awe na Elimu ya kidato cha nne (IV) au sita(VI) aliyehitimu mafunzo ya astashahada/stashahada (Diploma) katika fani zifuatazo:

I. Afya ya jamii (community healthy)
II. Fani ya uhusiano wa jamii (sociology)
III. AStashahada/Stashahada ya uuguzi (enrolled/registered nurse) lazima awe na leseni ya uuguzi iliyo hai ambayo imetolewa na Mamlaka husika.

### 2.2 SIFA ZA ZIADA / UZOEFU

Wenye uzoefu wa kuanzia mwaka mmoja au zaidi wa kufanya kazi ya ufuatiliaji wa huduma za wagonjwa majumbani pamoja na kliniki za tiba na matunzo (CTC).

### 2.3 KAZI / MAJUKUMU YA MFUATILIAJI WATEJA KATIKA KLINIKI ZA TIBA NA MATUNZO (CLINICAL TRACKER)

**I.** Kutambua wateja wanaokosa kufika vituo vya kutolea huduma kwa siku walizopangiwa na kufanya mawasiliano na wateja.

II. Kuchambua majalada ya wateja wenye sifa za kuchukuliwa kipimo cha wingi wa virusi (HVL).

III. Kuandaa na kuwasilisha Orodha ya wateja wasiopatikana kwa njia ya simu kwa wahudumu wa afya ngazi ya jamii kwa ajili ya kuwatafuta.

IV. Kufanya mawasiliano na wateja waliobainika na maambukizi ya VVU lakini hawafiki kwenye vituo vya kutolea huduma.

V. Kuhakikisha taarifa anazozitoa ziko sahihi katika mifumo ya kutolea taarifa (CTC 2 Database) pamoja na kutoa taarifa kila wiki kwenye mfumo wa kutolea taarifa.

VI. Kufanya kazi kwa kushirikiana na muuguzi mshauri, Msimamizi wa huduma za ukimwi ngazi ya jamii pamoja na Afisa takwimu kuhakikisha wateja waliohama kituo husika wanaendelea kupata huduma sehemu zingine.

VII. Kutoa elimu ya afya kwa familia juu ya umuhimu wa ufuasi mzuri wa mahudhurio ya kliniki ya tiba na matunzo.

VIII. Kuandaa taarifa za siku, wiki, mwezi pamoja na taarifa ya robo husika na kuziwasilisha kwa msimamizi wake ngazi ya wilaya.

IX. Kushiriki kikamilifu katika utunzaji wa takwimu katika kituo husika pamoja na vikao vya kutathimini takwimu katika ngazi ya wilaya.

X. Kufanya majukumu mengine atakayopangiwa na msimamizi wake wa kazi.

XI. Awe tayari kufanya kazi na kuishi katika mazingira yeyote hasa vijijini.

## 3.0 WAPIMAJI WA VVU KWA WENZA WA WAVIU (INDEX TESTERS) – NAFASI 2

### 3.1 SIFA ZA MWOMBAJI

I. Mwombaji anatakiwa awe na elimu ya kidato cha nne (IV) au sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya stashahada(Diploma)/shahada(degree) ya uuguzi.

II. Mwombaji lazima awe na leseni ya uuguzi iliyo hai ambayo imetolewa na Mamlaka husika.

### 3.2 SIFA ZA ZIADA

Mwombaji awe na uzoefu kuanzia mwaka mmoja au zaidi katika fani husika.

### 3.3 KAZI / MAJUKUMU YA WAPIMAJI WA VVU KWA WENZA

I. Kutoa elimu kwa wateja juu ya upimaji wa VVU.

II. Kutoa ushauri wa mara kwa mara pamoja na kutunza siri za wateja waliowahudumia.

III. Kuhakikisha anatoa msaada wa kuwaunganisha wateja waliobainika na maambukizi ya VVU ili waweze kuendelea kupata huduma katika vituo vya afya.

IV. Kuhakikisha hatua za upimaji zinafanyika kwa ufanisi kulingana na mwongozo wa taifa wa upimaji.

V. Kuhakikisha usalama wa upimaji wa wenza unafanyika kwa kuzingatia taratibu zote.

VI. Kutunza taarifa zote za upimaji wa wenza kwa ajili ya matumizi ya Ofisi.

VII. Kutunza takwimu za upimaji (HTS registers, reports and referral/linkage reports)

VIII. Kushirikiana na watumishi wengine katika kufuatilia mipango ya kuongeza ubora wa huduma katika viashiria vilivyowekwa

IX. Kufanya majukumu mengine atakayopangiwa na msimamizi wake wa kazi.

X. Awe tayari kufanya kazi na kuishi katika mazingira yeyote hasa vijijini.

## 4.0 TABIBU KATIKA KLINIKI YA TIBA NA MATUNZO (CLINICIAN) – NAFASI -1

### 4.1 SIFA ZA MWOMBAJI

I. Mwombaji anatakiwa awe na Elimu ya kidato cha nne (IV) au sita (VI) aliyehitimu mafunzo ya astashahada/stashahada (Diploma) katika fani ya udaktari.

II. Mwombaji lazima awe na leseni ya udaktari iliyo hai ambayo imetolewa na Mamlaka husika.

### 4.2 SIFA ZA ZIADA

Mwombaji awe na uzoefu kuanzia mwaka mmoja au zaidi katika fani husika.

### 4.3 KAZI / MAJUKUMU YA TABIBU WA KLINIKI YA TIBA NA MATUNZO

Mwombaji anatakiwa awe na ujuzi wa kisasa katika kutoa huduma za kitabibu kwa Watu wanaoishi na maambukizi ya VVU (WAVIU)

I. Kutoa huduma za kitabibu kwa WAVIU katika kliniki ya tiba na matunzo (CTC) ambazo ni pamoja na;
II. Matibabu ya magonjwa nyemelezi
III. Kufanya staging ya WAVIU, kuwaanzishia dawa za ARV, kuanzisha dawa siku husika (Same day initiation), kutoa dawa za miezi 3-6 kwa wateja wenye sifa na kuanzisha dawa kinga ya kifua kikuu (TPT initiation)
IV. Matibabu ya maudhi yatokanayo na dawa za ARV (ART complications)
V. Uanzishaji na ufuatiliaji wa dawa kinga ya VVU (Post Exposure Prophylaxis)
VI. Ujazaji sahihi wa kadi za CTC-2 na CTC-1, notisi za kitabibu na kutafsiri takwimu kwa ajili ya mipango mikakati ya kituo
VII. Kuandaa vikao vya ubora ili Kujadili mafanikio vs malengo na ubora wa huduma zitolewazo
VIII. Kutoa huduma/ushauri wa kitabibu kwa WAVIU waliolazwa wodini na katika idara ya magonjwa ya nje (OPD) kama itakavyohitajika
IX. Utunzaji sahihi wa taarifa za kitabibu na takwimu zingine zinazohijika kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini (monitoring and evaluation) ndani ya kliniki
X. Kuhudhuria vikao vya CTC na kusaidiana na Mfawidhi wa kituo katika mipango mikakati ya kliniki ya tiba na matunzo/ kliniki ya kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (CTC/PMTCT)
XI. Kufanya majukumu mengine atakayopangiwa na msimamizi wake wa kazi.
XII. Awe tayari kufanya kazi na kuishi katika mazingira yeyote hasa vijijini.

## MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE

i. Wawe raia wa Tanzania na wenye umri usiozidi miaka 45
ii. Waambatanishe vyeti vya kuzaliwa

iii. Waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (detailed CV) yenye anuani na namba ya simu za kuaminika.

iv. M aombi yote yaambatanishwe na picha 2 (passport size), nakala za vyeti vya taaluma, vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa zilizoelekezwa hapo juu.

v. "Testimonials", "Provisional Results", "Statement of Result", "hati za matokeo ya kidato cha nne na sita" (FORM IV AND FORM VI RESULT SLIP) **HAVITAKUBALIWA**

vi. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU, NACTE na NECTA)

vii. **Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 8 Novemba, 2021 saa 8:30 Alasiri.**

viii. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili HAYATAFIKIRIWA.

ix. Maombi yote yatumwe au yawasilishwe bayana katika masjala ya Mkurugenzi Mtendaji wilaya ya Nzega iliyopo eneo la Kampala- Ndala au kwa njia ya posta kwa anuani ifuatayo;-

**Mkurugenzi Mtendaji,**

**Halmashauri ya wilaya ya Nzega,**

**S.L.P 4**

**NZEGA.**

Kiomoni K. Kibamba

Mkurugenzi Mtendaji

**HALMASHAURI YA WILAYA**

**NZEGA**

MKURUGENZI
HALMASHAURI YA WILAYA
NZEGA.